Majukumu ya mfuko ni kubaini maeneo ya miradi ya mawasiliano ambayo yanaweza kupata ruzuku kutoka katika Mfuko; kuweka vigezo vya utambuzi wa maeneo ya vijiji vinavyohitaji na ambavyo haviwezi kupata huduma ya mawasiliano kwa sababu havina mvuto wa kibiashara na kuanzisha mfumo madhubuti wa usimamizi wa fedha za Mfuko.

Mfuko pia unaweka vigezo sahihi vya utoaji wa ruzuku kwa watoa huduma za Mawasiliano kwa ajili ya kupeleka mawasiliano katika maeneo yaliyoainishwa; unafanya tafiti mbalimbali na kufuatilia maendeleo ya mawasiliano katika maeneo ya vijijini na yale yasiyo na mvuto wa kibiashara na unatoa ushauri kuhusiana na mambo yanayohusu mawasiliano kwa wote.

Majukumu mengine ni kuangalia njia sahihi za kutoa ruzuku kwa ajili ya kupeleka huduma ya mawasiliano vijijini na katika maeneo yasiyo na mvuto kibiashara; kusimamia kisheria mikataba ya utekelezaji wa majukumu ya utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote na kuendesha na kuendeleza Mfuko kama ulivyoanzishwa.

Mfuko unaweka utaratibu mzuri wa kusimamia, kukokotoa na kukusanya tozo za Mawasiliano kwa wote kutoka kwa watoa huduma; unakokotoa, kupanga na kugawanya ruzuku za mawasiliano kwa wote na unapendekeza sera madhubuti za Mfuko kwa Waziri mwenye dhamana ya mawasiliano.

Pamoja na kusimamia miradi ya kufikisha mawasiliano kwa walengwa, Mfuko pia umetekeleza miradi mingine ikiwemo ya kufikisha matangazo ya runinga ya kidigitali; kuunganisha shule na mtandao wa intaneti, chini ya mradi unaojulikana kama *I-Knowledge*, kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu; tiba mtandao yaani *telemedicine* na ujenzi wa vituo vya TEHAMA.

Kupitia mradi wa kuunganisha shule, UCSAF kwa kushirikiana na kampuni binafsi iliyoshinda zabuni umewezesha vifaa vya TEHAMA na kuziunganisha na mtandao wa intaneti shule za umma 25, zikiwemo shule za watoto wenye mahitaji maalum.

Jedwali:
Mikoa na idadi ya vijiji vilivyofikiwa

Na.	Mkoa	Idadi
1	Arusha	69
2	Dar Es Salaam	3
3	Dodoma	164
4	Geita	122
5	Iringa	75
6	Kagera	98
7	Kaskazini Pemba (Pemba North)	3
8	Katavi	30
9	Kigoma	114
10	Kilimanjaro	31
11	Kusini Pemba (Pemba South)	3
12	Lindi	143
13	Manyara	143
14	Mara	36
15	Mbeya	197
16	Morogoro	195
17	Mtwara	137
18	Mwanza	13
19	Njombe	77
30	Pwani (Coast)	89
21	Rukwa	128
22	Ruvuma	169
23	Shinyanga	32
24	Simiyu	78
25	Singida	100
26	Tabora	163
27	Tanga	89
JUMLA		**2,501**

Shule 10 za watoto wenye mahitaji maalum zimepatiwa meza 10 na kompyuta 10 kila moja. Aidha shule nyingine 15 zilizobaki zimepatiwa kompyuta mbili kila moja pamoja na kuunganishiwa umemejua. Shule hizo zimeunganishwa kwenye intaneti.

Kwa upande wa mradi wa tiba mtandao, Mfuko umetoa pesa kwa ajili ya kukarabati vyumba vitakavyotumika kutolea huduma kupitia tiba mtandao katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili pamoja na kitengo cha MOI.

Mfuko pia umekuwa ukishiriki sherehe za Siku ya Wasichana na TEHAMA ambapo wasichana wa kidato cha tatu kutoka katika mikoa mbalimbali hupewa mafunzo maalum ya kutengeneza "application" za kompyuta.

Mpango wa siku ya Kimataifa ya Wasichana na TEHAMA ulianzishwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano (International Telecomunication Union, ITU) ili kuchochea uelewa juu ya masomo ya sayansi na hisabati na kuwawezesha na kuwahamasisha wasichana ili wachague mchepuo wenye fani ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Hii itawawezesha kupata na kutumia fursa zilizopo kwenye sekta ya TEHAMA. Siku hiyo inaadhimishwa Alhamisi ya nne ya kila mwezi Aprili.

Mradi wa *I-Knowledge* unalenga kuzipatia shule za sekondari na msingi vifaa vya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuziunganisha na mtandao wa intaneti, sambamba na utoaji wa mafunzo wa TEHAMA kwa walimu wa shule hizo.

Shule 300 ikiwa ni mchanganyiko wa za sekondari na msingi nchini kote zimefaidika na mradi huo.

Mfuko umetoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu katika shule mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kutatua matatizo madogo madogo ya vifaa vya TEHAMA vilivyopo mashuleni mwao, ambavyo vimetolewa ama na Mfuko au na wadau wengine. Mwaka 2016/17, mafunzo yalitolewa kwa walimu 286, na 2017/18 kwa walimu 297.

Mfuko umejenga vituo 10 vya TEHAMA Pemba na Unguja ambavyo vinatoa huduma mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kudurufu nyaraka mbalimbali, kupiga simu, kutoa huduma za kutuma na kupokea fedha pamoja na mafunzo.



Uzinduzi wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa TCRA, uliofanyika mjini Dodoma, ulihudhuriwa na wadau mbalimbali, na wengi: wakiwemo mawaziri, wabunge, watoa huduma, watumiaji na wananchi.

TCRA yainua vigezo ubora huduma zake

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imezindua mkataba wake kwa wateja, ukiwa na malengo ya kuboresha huduma ikiwa ni pamoja na kupunguza muda wa kupata leseni kuwa kati ya siku 14 na 60. Mkataba huo, uliozinduliwa hivi karibuni mjini Dodoma, unarejea azma ya Mamlaka ya kutoa huduma kwa usawa, ufanisi na uwazi zaidi. TCRA ina viwango vya utoaji huduma vya ISO 9001:2015. Mkataba huo unatolewa hapa kwa urefu.

UTANGULIZI

MKATABA wa Huduma kwa Mteja wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ambacho ni kifupi cha Tanzania Communications Regulatory Authority umeandaliwa kwa lengo la kufafanua sisi ni nani, wadau wetu, wateja wetu, huduma zetu na viwango vya utoaji huduma. Mkataba huu unaakisi dhamira ya dhati ya TCRA ya kuwahudumia wateja bila ya upendeleo, kwa uaminifu, kwa heshima, katika viwango vilivyoainishwa na kwa muda unaokubalika.

Mkataba huu umekusudia kuboresha utoaji wa huduma kwa kutoa taarifa kuhusu TCRA, kuwapatia wadau uelewa kuhusu huduma zetu za msingi na viwango vya huduma tunazotoa.

Mkataba huu unaainisha nia ya TCRA ya kuimarisha utendaji na utoaji huduma

bora kwa wadau na umma kwa lengo la kumridhisha mteja kulingana na mahitaji na matarajio yake. Aidha, Mkataba huu unaonesha vizuri kiwango cha uwazi, pamoja na haki na wajibu wa wateja wetu.

Ni utashi na kiu yetu kuona kuwa wakati tunatoa huduma, mteja anapata fursa ya kutupima kama tumefikia viwango vilivyooneshwa katika Mkataba huu na hivyo tungependa na kufurahi kupata mrejesho wake kuhusu huduma zetu. Iwapo huduma zetu zitakuwa chini ya viwango vilivyowekwa, hatua za kuchukua na kufanya marekebisho zimewekwa ili tuendelee kuboresha huduma zetu na kukidhi mahitaji ya wateja na wadau wote.

Kwa sasa, TCRA inayo Ofisi yake Zanzibar na imeunda Kanda tano (5) kama ifuatavyo: - (i) Kanda ya Mashariki (**DAR ES SALAAM**, Mtwara, Lindi, Pwani na Morogoro) (ii) Kanda ya Kaskazini (**ARUSHA**, Kilimanjaro, Tanga na Manyara) (iii) Kanda ya Kati (**DODOMA**, Singida, Tabora na Kigoma) (iv) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini **(MBEYA,** Ruvuma, Iringa, Njombe, Rukwa, Songwe na Katavi) (v) Kanda ya Ziwa (**MWANZA**, Shinyanga, Geita, Mara, Simiyu na Kagera).

SISI NI NANI

TCRA ni Taasisi ya Serikali ya Udhibiti, yenye wajibu wa kusimamia na kuendeleza mawasiliano ya simu, intaneti, maudhui ya utangazaji (redio na televisheni) na huduma za posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto.

Dira yetu

Kuwa Mdhibiti wa Mawasiliano ya Posta na Kielektroniki mwenye hadhi ya kimataifa.

Dhamira yetu

Kusimamia huduma za Mawasiliano ya Posta na Kielectroniki kwa ufanisi; kuboresha utendaji wa watoa huduma na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano kwa lengo la kutoa mchango wetu kwa maendeleo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sera ya Ubora wa Huduma Zetu

TCRA imejikita katika kuboresha ustawi wa Watanzania kupitia utoaji wa huduma za udhibiti zenye ubora ambazo zitahakikisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa wote na kwa kutekeleza mfumo wa ubora wa uendeshaji katika shughuli zote.

TCRA inaboresha na kupitia upya malengo yake ya ubora mara kwa mara na kuwafahamisha wahusika wote ndani ya Mamlaka.

Lengo Kuu

Kuboresha maisha ya Watanzania kupitia udhibiti wenye ufanisi, unaochochea na kukuza ubunifu na ambao unahakikisha kupatikana kwa huduma bora na imara za Mawasiliano ambazo zinatolewa kwa gharama nafuu.

Maadili ya Msingi

Watumishi wa TCRA wamelelewa katika maadili ambayo yanazingatia na kuhakikisha kuwa dira na dhamira zinafikiwa na hatimaye mteja kuridhika na huduma zetu. TCRA itaongozwa na itazingatia nguzo kuu zifuatazo:

Utalaam: Tunadumisha kiwango cha juu cha utalaam, weledi na maadili ili kujenga uhusiano wa ongezeko la thamani kwa wateja na wadau ili kutoa huduma bora.

Heshima: TCRA inawathamini wafanyakazi na kuwaheshimu wateja na wadau wake.

Uwezeshaji:Tunaamini katika kuwawezesha na kuwapa wafanyakazi uwezo wa kupambana na changamoto, kutoa maamuzi na kutekeleza kikamilifu wajibu wao katika sehemu zao za uwajibikaji.

Ubunifu: Tunahimiza ubunifu na uvumbuzi unaolenga kuongeza uwezo na ufanisi katika kushughulikia masuala ya udhibiti.

Uadilifu: Tunaamini katika uadilifu na tunakusudia kuwahudumia wateja na wadau wote kwa uadilifu, usiri na uaminifu.

Uwajibikaji: Tunawajibika, katika kutekeleza majukumu yetu kwa haki, kujali na kwa kuzingatia dhana ya uwazi.

Utendaji wa Pamoja: Tunanufaika na utendaji kazi wa pamoja na kutumia hazina ya utaalamu uliopo ili kupata mafanikio.

Ufanisi: Tunaamini katika kutoa huduma za udhibiti kwa ufanisi na kutafuta fursa zaidi ili kuongeza huduma zetu.

Kutokuwa na Ubaguzi: Tunaamini katika fursa sawa katika kuwahudumia wadau wa ndani na nje bila ya ubaguzi wa aina yoyote ile.

KUSUDIO LA MKATABA HUU

Mkataba huu unakusudia kuongeza uelewa wa wadau kuhusu TCRA, huduma tunazotoa, haki na wajibu wa wateja wake na jinsi ya kuhamasisha wadau wasioridhika na huduma zetu kuwasilisha malalamiko yao.

Aidha, Mkataba huu unakusudia kuwafanya watumishi wa TCRA kuwa na mtazamo wa kujali na kuheshimu zaidi mahitaji ya wateja na wadau wote.

MALENGO MAKUU YA KIMKAKATI

Mkataba huu wa Huduma kwa Mteja wa TCRA umezingatia malengo mkakati sita (6) kama yalivyoainishwa katika Mpango Mkakati wa miaka mitano (5) (2016/17-2020/21).

Malengo haya ni:

(i) Kuzifanya shughuli za TCRA kuwa za kisasa kwa kutumia teknolojia sahihi; kuimarisha tafiti zenye ubora katika huduma zinazodhibitiwa, uwezo na umahiri wa watumishi.

(ii) Kukuza ufanisi; kuaminika na kuhakikisha usalama wa miundombinu ya mawasiliano na matumizi yake.

(iii) Kukuza ufanisi na unafuu wa huduma za Mawasiliano na kuongeza upatikanaji wa huduma za Posta na TEHAMA katika maeneo yasiyohudumiwa ipasavyo na yale yasiyo na huduma kabisa. (iv) Kulinda maslahi ya wadau na kukuza uelewa wa haki na wajibu wao.

(v) Kufuatilia utendaji wa huduma zinazosimamiwa na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria na Kanuni kwa viwango vinavyostahili.

(vi) Kuratibu utekelezaji wa ahadi za kisekta kitaifa, kikanda na kimataifa.



Mwananchi akiwa na machapisho ya TCRA baada ya kupata huduma kwenye banda la Mamlaka wakati wa kampeni iliyofanyika Morogoro kuhusu usajili wa laini za simu.

WADAU WETU

Wafuatao ni wadau wetu wakuu: -

(i) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(iii) Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(iv) Baraza la Wawakilishi Zanzibar;

(v) Idara za Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(vi) Wawekezaji na watoa huduma katika sekta za mawasiliano;

(vii) Tume ya Ushindani (FCC);

(viii) Baraza la Ushindani la Taifa (FCT);

(ix) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote

(UCSAF);
(x) Watumiaji wa huduma za mawasiliano;
(xi) Baraza la Ushauri la watumiaji huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC);
(xii) Mamlaka za Usimamizi na Udhibiti;
(xiii) Taasisi na Asasi zinazohusiana na sekta ya Mawasiliano kimataifa;
(xiv) Vyombo vya Ulinzi na Usalama;
(xv) Watumishi wa TCRA;
(xvi) Taasisi za Elimu na utafiti;
(xvii) Mahakama;
(xviii) Wananchi;
(xix) Vyombo vya Habari;
(xx) Asasi za Kiraia; na
(xxi) Washirika wa kimaendeleo.

WAJIBU, MAJUKUMU NA KAZI ZETU

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilianzishwa kwa Sheria ya TCRA Na. 12 ya Mwaka 2003 kufuatia kuunganishwa kwa zilizokuwa Tume ya Mawasiliano Tanzania (TCC) na Tume ya Utangazaji Tanzania (TBC). Wajibu na kazi kuu za TCRA ni: -

(i) Kuweka mazingira sawa ya utendaji kazi ili kuimarisha ushindani wa haki na kukuza maendeleo ya kiuchumi;
(ii) Kulinda maslahi ya wateja;
(iii)Kuendeleza uwepo wa huduma zinazodhibitiwa;
(iv)Kutoa leseni na kusimamia masharti ya leseni za uendeshaji wa huduma za utangazaji, posta na mawasiliano ya simu;
(v)Kuweka na kusimamia viwango vya bidhaa na huduma zinazosimamiwa;
(vi)Kudhibiti viwango vya gharama na tozo za mawasiliano;
(vii)Kusimamia rasilimali masafa na namba zinazotumika katika utoaji wa huduma za mawasiliano ya simu; na
(viii)Kusimamia utendaji wa sekta zinazodhibitiwa.

AHADI KWA MTEJA KATIKA UTOAJI WA HUDUMA

Katika kutekeleza wajibu wetu kisheria, TCRA tunaahidi wateja kuwa: -

(i) Tutahakikisha wateja wetu wanapata huduma bora, kwa ufanisi, katika wakati unaokubalika na viwango vilivyowekwa;
(ii) Tutatoa huduma zetu pasipo kudai au kupokea rushwa ama kutoa upendeleo wa kibaguzi au kinyume na Sheria, Kanuni, Miongozo, na Taratibu;
(iii) Tutahakikisha tunaendelea kuwa na heshima na kauli nzuri kwa wateja;
(iv) Tutazingatia kikamilifu Mwongozo wa Maadili wa TCRA.
(v)Tutaondoa mapungufu ya kiutendaji mara pale yanapojitokeza au kubainishwa;
(vi) Tutaendelea kutoa elimu kwa wadau, wateja wetu na umma kuhusu huduma zetu, haki na wajibu wao;
(vii) Tutashirikisha kila mara wateja na wadau wa sekta ya Mawasiliano katika mashauriano ya kuboresha huduma zetu;
(viii) Tutazingatia viwango vya huduma ambavyo tunaahidi na kufuatilia, kutathimini utendaji na kupima matokeo;
(ix) Tutatoa taarifa sahihi za kuaminika kuhusu mabadiliko ya huduma mara yatakapotokea.

AINA ZA LESENI ZETU

(A) Mfumo Kutaniko wa Utoaji wa Leseni (Converged Licensing Framework - CLF) wenye sehemu nne za soko zinazoitwa; Kimataifa, Kitaifa, Kimkoa na Kiwilaya.

Hizi ni leseni Kutaniko ambazo zina teknolojia na huduma huru kama zinavyooelezwa hapa chini:

1. Leseni ya Vifaa vya Miundombinu (Network Facilities Licence – NFL); inaidhinisha, umiliki, udhibiti na ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano ya kielektroniki.
2. Leseni ya Huduma za Miundombinu (Network Services Licence - NSL) – inatoa idhini ya kuendesha na kumiliki mitandao ya mawasiliano ya kielektroniki ili kutoa huduma.
3. Leseni ya Matumizi ya Huduma (Application Services Licence - ASL) – inaidhinisha utoaji wa huduma za kielektroniki kwa wateja wa mwisho.
4. Leseni ya Huduma ya Maudhui (Content Services Licence - CSL) – inaidhinisha utoaji wa maudhui kama vile utangazaji kwa njia ya Satelaiti na Utangazaji huru kwa njia ya miundombinu ya ardhini wa redio na vyombo vingine vya habari vya kielektroniki.
5. Leseni ya Huduma ya Maudhui kwa Mtandao (Online Content Licence) – inaidhinisha utoaji wa maudhui kwa njia ya mtandao.



Baadhi ya wataalam wa TCRA na wa wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano waliohudhuria mafunzo mafupi mjini Bagamoyo hivi karibuni **kuhusu teknolojia mpya za mitandao (new emerging technologies); yaliyotolewa na Shirika la Mawasiliano la Jumuia ya Madola (CTO).** ***Waliokaa ni Mkurugenzi wa TEHAMA wa Mamlaka, Connie Francis (katikati),*** **ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu kwenye ufunguzi wa mafunzo hayo;** ***Mkuu wa*** **Utumishi na Utawala,TCRA** ***Bw. Erasmo Mbilinyi (kushoto) na mkufunzi, Bw.*** **Sunjay Kumar kutoka BSNL India, aliyeendesha msfunzo hayo kwa niaba ya CTO.**

(B) Leseni Nyingine

Kuna makundi mengine ya leseni zinazotolewa na TCRA ambayo hayamo kwenye Mfumo Kutaniko wa Utoaji wa Leseni (CLF). Makundi haya yanajumuisha:

(i) Leseni ya Ufungaji na Matengenezo ya Vifaa vya Mawasiliano;

(ii) Leseni ya Uingizaji wa Vifaa vya Mawasiliano;

(iii) Leseni ya Usambazaji wa Vifaa vya Mawasiliano;

(iv) Leseni ya Uuzaji wa Vifaa vya Mawasiliano;

(v) Leseni ya Huduma za Posta na Usafirishaji wa vipeto na vifurushi; (vi) Leseni ya Huduma ya Ujumbe Mfupi;

(vii) Leseni ya Matumizi ya Masafa ya Mawasiliano ya Redio;

(viii) Leseni ya Ungo (VSAT);

(ix) Leseni ya Kutoa Namba na Anwani za kielektroniki;

(x) Leseni ya Mawasiliano ya Redio;

(xi) Leseni ya Huduma ya Kuthibitisha Ubora wa Vifaa vya Mawasiliano kwa ajili ya matumizi nchini.

VIWANGO VYA HUDUMA ZETU

Hizi ni ahadi ambazo tunazitoa kwa watumiaji wa huduma kuhusu viwango na ubora wa huduma wanazoweza kutarajia. Tunaahidi kutoa huduma za viwango vya juu kupitia Mkataba huu unaolenga kuboresha huduma kwa wateja wetu.

Lengo la TCRA ni pamoja na kuweka viwango vya juu vya huduma na kuweka uwezekano wa kupima, kiwango chetu cha uwajibikaji katika kutoa huduma. Tuna maadili na viwango vya utendaji wa huduma kwa mteja ambavyo wafanyakazi wetu wanatakiwa kuvizingatia katika utendaji wao.

Unapokuwa Unashughulika nasi, tegemea mambo yafuatayo: -

(i) Kukutana na watu wenye ukarimu, adabu, heshima na kuhudumiwa kwa haki;

(ii)Tutakuhudumia kwa unyenyekevu na kuwasiliana nawe vizuri wakati wote;

(iii)Tutakuarifu huduma tunayoweza kukupatia, jinsi ya kupata na mhusika wa kuwasiliana naye;

(iv)Tutakupatia taarifa zenye ubora unaofaa kwa mahitaji yako;

(v)Tutahakikisha tunatoa huduma bora zinazokidhi matarajio yako;

(vi)Tutakupatia vipindi halisi vya utoaji huduma kuhusiana na aina ya maombi; (vii)Tutapima utendaji wetu kwa dhana ya "kilicho bora katika biashara."

Kipindi cha huduma zetu

(a) Shughuli na Vigezo vya Utendaji

(i)Mawasiliano	
Shughuli	**Viwango vya Utendaji**
Ukitembelea Ofisini, huduma katika Kaunta ya Mapokezi	Ndani ya Dakika kumi na tano (15)
Kupokea simu	Ndani ya Miito sita (6) ya kwanza
Kujibu maulizo, vyombo vya habari na wadau wengine wote	Ndani ya Siku tano (5) za kazi baada ya kupokelewa
Kujibu Maombi ya Leseni kwa mteja	Ndani ya siku mbili (2) za kazi baada ya kupokelewa
Kukiri kupokea Barua pepe (@tcra. go.tz), Nukushi, Mitandao ya kijamii (twiter, facebook instagram)	Ndani ya Saa 24 baada ya kupokelewa
(ii) Kushughulikia malalamiko	
Shughuli	**Viwango vya Utendaji**
Kukiri kupokea malalamiko	Ndani ya Siku tatu (3) za kazi
Kumfahamisha Mtoa huduma aliyelalamikiwa	Ndani ya Siku tano (5) za kazi tangu kupokelewa kwa malalamiko
Mrejesho wa mwenendo wa uchunguzi wa malalamiko	Ndani ya Siku kumi na nne (14) za kazi tangu kupokelewa
Kufanya vikao vya usuluhishi wa malalamiko inapohitajika	Ndani ya Siku sitini (60) tangu kujaza fomu ya malalamiko.
Kukamilisha na kutoa uamuzi wa malalamiko	Ndani ya Siku sitini (60) za kazi tangu kufanyika kikao cha usuluhishi
Kutoa kumbukumbu za mwenendo wa shauri na hukumu	Ndani ya Siku saba (7) baada ya kutolewa kwa hukumu/ maamuzi
(iii) Kupitia na Kutoa Kibali cha Mabadiliko ya bei za Mawasiliano	
Shughuli	**Viwango vya Utendaji**
Kukiri kupokea maombi ya mabadiliko ya bei	Ndani ya siku tatu za kazi
Mkutano na mwombaji kuhusu mabadiliko yaliyopokelewa	Ndani ya Siku kumi na nne (14) za kazi tangu kupokelewa
Kutoa uamuzi wa maombi ya mabadiliko ya bei	Ndani ya Siku thelathini (30) za kazi tangu kupokelewa
(iv) Utoaji Wa Leseni	
Shughuli	**Viwango vya Utendaji**
Upitiaji wa mwanzo wa maombi na kutoa barua kuhusu maombi (mrejesho wa awali)	Ndani ya Siku Siku tano (5) za kazi

Kufanya ukaguzi pale inapotakiwa	Ndani ya Siku tano (5) baada ya barua ya mrejesho wa awali
Kutoa kibali cha ujenzi wa muundombinu pale inapotakiwa	Ndani ya Siku kumi na nne (14) za kazi baada ya ukaguzi
Kutoa Leseni ya kujenga Miundombinu ya mtandao wa mawasiliano	Ndani ya Siku sitini (60) za kazi tangu kupokelewa
Kutoa Leseni ya Huduma ya Mtandao	Ndani ya Siku sitini (60) za kazi tangu kupokelewa
Kutoa Leseni ya Matumizi ya Huduma za mtandao	Ndani ya Siku sitini (60) za kazi tangu kupokelewa
Kutoa Leseni ya kutoa maudhui ya Utangazaji	Ndani ya Siku sitini (60) za kazi tangu kupokelewa
Kutoa Leseni ya utoaji wa maudhui Mtandaoni	Ndani ya Siku kumi na nne (14) za kazi tangu kupokelewa
Kutoa Leseni ya Kusimika na kurekebisha Mitambo ya mawasiliano	Ndani ya Siku Siku thelathini (30) za kazi tangu kupokelewa
Kutoa Leseni ya Uingizaji, usambaji na uuzaji wa vifaa vya mawasiliano	Ndani ya Siku saba (7) za kazi tangu kupokelewa
Kutoa Huduma za Posta na Usafirishaji vipeto	Ndani ya Siku thelathini (30) za kazi tangu kupokelewa
Kutoa Huduma za Ujumbe Mfupi	Ndani ya Siku saba (7) za kazi tangu kupokelewa
Kutoa Matumizi ya Masafa na Mawasiliano ya Redio	Ndani ya Siku saba (7) za kazi tangu kupokelewa
Kutoa huduma ya Kusimika na Kutumia VSAT	Ndani ya Siku saba (7) za kazi tangu kupokelewa
Kutoa Namba na Anwani za Kielektroniki	Ndani ya Siku saba (7) za kazi tangu kupokelewa
Kuthibitisha Ubora wa Vifaa vya Mawasiliano kwa ajili ya matumizi hapa nchini	Ndani ya Siku kumi na nne (14) za kazi tangu kupokelewa
(v) Ufuatiliaji na Ukaguzi wa wenye Leseni	
Shughuli	**Viwango vya Utendaji**
Kujibu taarifa za kila robo mwaka zinazopokelewa kwa mujibu wa Kanuni	Ndani ya Siku saba (7) za kazi tangu Kupokelewa
Kupitia na Kujibu Mpango Mkakati wa biashara (business Plans) zinazopokelewa kwa mujibu wa Kanuni	Ndani ya Siku kumi na nne (14) za kazi tangu kupokelewa
Kutoa mrejesho wa ukaguzi ambao umefanyika kwa mtoa huduma aliyekaguliwa	Ndani ya Siku kumi na nne (14) za kazi tangu kukamilika kwa ukaguzi

(vi) Utoaji wa habari	
Shughuli	**Viwango vya Utendaji**
Utoaji wa uamuzi wa bei za muingiliano mitandao ya simu kwenye Gazeti la Serikali	Ndani ya Siku saba (7) baada ya uamuzi
Kutoa taarifa kwa wafanyakazi kuhusu maamuzi muhimu ya Menejimenti, Bodi ya Wakurugenzi na Serikali	Ndani ya Siku tatu (3) za kazi baada ya maamuzi
Kutoa taarifa za Mpango wa Mwaka wa Manunuzi	Ndani ya Siku thelathini (30) kabla ya mwaka mpya wa fedha kuanza
Kuwasilisha Mikataba ya Zabuni kwa Mwanasheria Mkuu	Ndani ya Siku saba (7) baada ya maamuzi ya Bodi ya Tenda
Kuwasilisha marejeo ya Mkataba wa Utendaji kwa Msajili wa Hazina	Ndani ya Siku tano (5) baada ya maamuzi ya Bodi
Kuchapisha Taarifa ya Mwaka ya Utendaji ya TCRA	Ndani ya Siku mia moja na themanini (180) za Kazi baada ya kukamilika ukaguzi
(vii) Malipo kwa Wateja wa Ndani	
Shughuli	**Viwango vya Utendaji**
Kukamilisha maombi ya malipo	Ndani ya Siku saba (7) za kazi tangu kuidhinishwa
Kuingiza kumbukumbu za malipo	Ndani ya Siku mbili (2) za kazi tangu kupokelewa
Kusaini hundi ya malipo	Ndani ya Siku mbili (2) za kazi baada ya kuandikwa
Kumfahamisha kwa barua pepe au simu mtumishi kuhusu kukamilika kwa malipo yake	Ndani ya Siku mbili (2) tangu kukamilika
Kutoa taarifa ya mshahara	Ndani ya siku moja (1) baada ya mshahara kupelekwa benki
(viii) Malipo kwa Wateja wa Nje	
Shughuli	**Viwango vya Utendaji**
Kuidhinisha maombi ya malipo	Ndani ya Siku tano (5) za kazi
Kukamilisha maombi ya malipo yasiyo ya manunuzi	Ndani ya siku saba (7) za kazi tangu kupokelewa
Kuingiza kumbukumbu za malipo	Siku mbili (2) za kazi tangu kukamilika
Kusaini hundi ya malipo	Siku mbili (2) za kazi tangu kukamilika
Kumfahamisha kwa barua pepe au simu mlipwaji kuhusu kukamilika kwa malipo yake	Siku mbili (2) tangu kukamilika
Malipo kwa watoa huduma kwa TCRA	Sawa sawa na ilivyo katika Mkataba wa manunuzi



Afisa wa TCRA, Judith Shao akihudumia watumiaji wa huduma za mawasiliano kwenye kampeni ya elimu kwa umma iliyofanyika Morogoro hivi karibuni.

(b) Siku za kazi ni Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 2:00 (mbili) asubuhi hadi saa 10:00 (kumi) jioni.

(c) Kutakuwepo na dawati la msaada kwa wateja (Help-Desk) la kutoa huduma kwa mteja ambae hahitaji kumwona ofisa.

(d)Tutajitambulisha kwa kuonyesha kitambulisho cha kazi.

(e) Mgeni au mteja utasindikizwa na kukabidhiwa kwa Ofisa anayehusika kwa suala lako.

(f) Malalamiko yote halali yatawekwa katika daftari (register) siku yanapopokelewa.

Msingi wa Ufanisi katika Kushughulikia Malalamiko

Mchakato wetu utazingatia mambo yafuatayo:

(i) Haki ya msingi ya kusikilizwa;

(ii) Kuwasilishwa kwa malalamiko husika;

(iii)Malalamiko kuwa katika lugha ya Kiingereza au Kiswahili;

(iv)Kuwapo utaratibu rahisi kuelewa na kutumia;

(v) Malalamiko yatashughulikiwa kwa muda uliokubalika;

(vi)Kuhakikisha uchunguzi kamili na wa haki wa malalamiko;

(vii) Kuheshimu matakwa ya watu kwa ajili ya usiri;
(viii) Kueleza hoja zote kwa wakati, kutoa majibu na marekebisho yanayofaa.

Kuwajibika katika Utoaji Huduma

TCRA inawajibika kukuhudumia kwa wakati, kwa kuzingatia uadilifu, uaminifu, haki, ufanisi na ubora. Hatutatoa motisha kwa namna ya zawadi au upendeleo kwa wafanyakazi wetu au kuwashawishi ili watoe huduma.

Aidha, tutaendelea kuelimisha wateja na umma kuhusu viwango vya utoaji wa huduma zetu.

Utaratibu wa Malalamiko

Wateja wanahamasishwa kuleta malalamiko kwa Mkurugenzi Mkuu kwa kufika, kwa simu, kwa maandishi, barua pepe, mitandao ya kijamii - twitter@TCRA_TZ,@ TCRA1, au nukushi +255 22 2412009 -10.

(i) Malalamiko ya jumla yatumwe kupitia anwani ya barua pepe - malalamiko@tcra.go.tz au kwa kupiga simu namba +255 22 2412011 - 2; +255 22 2199760-9.

(ii) Kituo cha Huduma kwa Wateja (Call Centre) 0800 008272, +255 22 2008272.

(iii) Malalamiko yanayohusiana na vitendo vya rushwa yawasilishwe kupitia anwani ya barua pepe - norushwa@tcra.go.tz au kwa kupiga simu namba +255 737 300300.

(iv)Tutahakikisha usiri na faragha kwa kuheshimu utambulisho wa mlalamikaji na kiini cha malalamiko ili kulinda haki ya wateja. Hata hivyo, tunawahamasisha walalamikaji kujibainisha wenyewe kutokana na ugumu wa kiutendaji kushughulikia malalamiko yasiyo na jina.

Haki kwa Mteja wetu

(i) Kuhudumiwa kwa viwango vilivyowekwa.
(ii) Kufanya mapitio na kukata rufaa dhidi ya uamuzi wetu.
(iii) Kuwasilisha malalamiko kuhusu huduma za TCRA.
(iv) Kupata kumbukumbu za mwenendo wa shauri lililowasilishwa katika Kamati ya Malalamiko na hukumu iliyotolewa.
(v) Kupata huduma bila ubaguzi kama vile rangi, dini, elimu, ukanda, kabila, ulemavu, jinsia na mafungamano yoyote.
(vi) Kupata taarifa sahihi na kwa wakati kulingana na Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.
(vii) Kupata faragha na usiri katika masuala yanayowasilishwa.

Wajibu wa Mteja

TCRA inatarajia yafuatayo toka kwa wateja wetu:
(a) Kuthamini huduma zetu;
(b) Kulipia leseni kwa wakati unaohitajika;
(c)Kutoa mapendekezo ya kuboresha huduma zetu kwa njia ya barua, maoni kwenye sanduku, barua pepe au simu;
(d) Kuzifahamu huduma zetu;
(e)Kutoa taarifa sahihi, nyaraka au viambatanisho kamili;
f) Kufahamu vizuri Sheria, Kanuni, miongozo na taratibu zetu;
(g)Kuwasilisha taarifa kamili na sahihi kutuwezesha kuchukua hatua zinazostahili;
(h) Kubainisha maeneo ya udhaifu katika utoaji wa huduma zetu;
(i)Kushiriki katika programu zetu za uhamasishaji na ushirikishwaji;
(j) Kutunza mazingira;
(k) Kutunza miundombinu ya Mawasiliano;
(l) Kufuata Sheria zinazoongoza matumizi ya huduma za mawasiliano.

MAPITIO NA MAREKEBISHO YA MKATABA

Kuzingatia mazingira yanayobadilika, kwa kushauriana na wateja/wadau, tutafanya mapitio ya Mkataba huu kwa Mteja kwa lengo la kuboresha huduma zetu.

MREJESHO WA UTOAJI HUDUMA ZETU

Tutafurahi kupata mrejesho wa namna tunavyotoa huduma zetu. Unaweza kuwasiliana nasi kuhusu huduma zetu kwa kutumia sanduku la maoni au kuandika barua au barua pepe kwenda Makao Makuu, Ofisi ya Zanzibar na Ofisi za Kanda kwa anwani zilizotolewa hapa chini:

Makao Makuu: Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Mawasiliano Towers 20 Barabara ya Sam Nujoma, S.L.P 474 14414 DAR ES SALAAM. Simu : +255 22 2199760 - 9 +255 22 2412011 - 2 +255 784558270 - 1 Nukushi : +255 22 2412009 -10. Baruapepe : dg@tcra.go.tz Tovuti : www.tcra.go.tz

Ofisi ya Zanzibar: Mkuu wa Ofisi ya TCRA 19 Mtaa wa Mbuyukisutu, S.L.P 3284 71194 Mjini Magharibi, ZANZIBAR. Simu: +255 24 223 5062. Baruapepe: zanzibar@tcra.go.tz

Ofisi ya Kanda ya Mashariki: Mkuu wa Kanda, 147 Barabara ya Kajenge, S.L.P 35615 14194 DAR ES SALAAM. Simu : +255 22 2775110 +255 22 2775114. Baruapepe: easternzone@tcra.go.tz.

Ofisi ya Kanda ya Kati: Mkuu wa Kanda, Jengo la LAPF, Ghorofa ya 4, 2 Mtaa wa LAPF, S.L.P 2229 41194 DODOMA. Simu : +255 26 232 1731. Baruapepe: dodoma@tcra.go.tz

Ofisi ya Kanda ya Ziwa: Mkuu wa Kanda, Jengo la NSSF Mafao, Ghorofa ya 4, Wing B, 13 Barabara ya Jomo Kenyatta S.L.P 3108 33194 MWANZA. Simu: +255 28 2505082. Baruapepe: mwanza@tcra.go.tz

Ofisi ya Kanda ya Kaskazini: Mkuu wa Kanda, Jengo la Summit Centre, Ghorofa ya 3, Block B 103 Barabara ya Sokoine, S.L.P 15675 23194 ARUSHA. Simu: +255 27 254 8947. Baruapepe: arusha@tcra.go.tz

Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini: Mkuu wa Kanda, Jengo la Century Plaza, Ghorofa ya 1, Barabara ya Tunduma, P. O. Box 1375 53194 MBEYA. Simu: +255 25 250 5016. Baruapepe: mbeya@tcra.go.tz



Mkazi wa Iringa akipitia mwongozo wa watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano ambao, pamoja na mambo mengine, unaelezea haki na wajibu wa watumiaji.

MANUFAA YA MATUMIZI YA POSTIKODI



Mfumo wa postikodi una manufaa mbalimbali kwa Serikali, watoa huduma za posta, wafanyabiashara, jamii na taasisi zisizo za kiserikali; manufaa haya ni ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa maendeleo ya taifa.

- Ni msingi wa kutoa utambulisho wa eneo maalumu kama Kata au Wadi;
- Unaongeza ufanisi katika utoaji wa huduma katika makazi ya watu;
- Unaongeza tija kwenye huduma za uokoaji na maafa;
- Unawezesha ukusanyaji wa kodi mbalimbali kwa urahisi na kwa wakati;
- Ni chanzo cha mapato yatokanayo na maombi ya orodha ya postikodi kwa ajili ya shughuli za utafiti na biashara; na
- Unaongeza kasi ya kupambana na uhalifu, kuimarisha shughuli za uhamiaji, utalii, ulinzi na usalama.
- Unarahisisha uchambuaji wa barua na vifurushi kuwa wa haraka na ufanisi zaidi;
- Unaongeza ufanisi katika usafirishaji na usambazaji
- wa barua na vifurushi;
- Unawezesha utambuzi wa anwani kuwa rahisi zaidi;
- Unaongeza ufanisi katika kushughulikia malalamiko ya wateja;
- Unapunguza uwezekano wa barua na vifurushi kupotea; na
- Ni chanzo cha mapato yatokanayo na kuunganishwa na Hifadhi–Data ya Postikodi.
- Unawezesha biashara mtandao na upatikanaji wa huduma nyingine za kijamii kama vile za afya na usalama;
- Unawezesha kutambua eneo kirahisi na kufahamu mahali alipo mtu au kitu hivyo kupunguza muda na gharama za usafiri; na
- Unarahisisha upatikanaji wa takwimu kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali za maendeleo ya kijamii.
- Unaboresha utafiti wa maendeleo ya biashara;
- Unarahisisha upatikanaji wa takwimu kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali za maendeleo ya kibiashara.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

ISO 9001:2015 CERTIFIED

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania(TCRA) ni taasisi ya Serikali inayosimamia sekta ya mawasiliano. TCRA ilianzishwa chini ya Sheria ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania Na 12 ya 2003. TCRA ina viwango vya ISO 9001:2015.



Maeneo yanayosimamiwa

Mitandao ya simu na intaneti, masafa ya mawasiliano,huduma za Posta na usafirishaji wa vipeto katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na huduma za utangazaji (kama vile redio na televisheni) kwa Tanzania Bara tu. Zanzibar ina Tume inayosimamia utangazaji.

Kazi za TCRA

- Kutoa leseni, kuongeza muda wa leseni na kufuta leseni
- Kuweka viwango kwa bidhaa na huduma zinazosimamiwa
- Kuweka viwango vya kanuni na masharti ya kusambaza bidhaa na huduma zinazosimamiwa
- Kudhibiti viwango na bei
- Kufuatilia utendaji wa sekta ya mawasiliano kuhusiana na viwango vya uwekezaji; upatikanaji wa huduma, ubora na viwango vya huduma; gharama za huduma; ufanisi wa bidhaa na usambazaji wa huduma.
- Kufanikisha utatuzi wa malalamiko na migogoro baina ya watoa huduma na kati ya mtoa huduma na mtumiaji wa huduma.
- Kufanya kazi na kutekeleza majukumu mengine kwa mujibu wa sheria husika
- Kusambaza taarifa kuhusu mambo ambayo ni muhimu kwa ajili ya shughuli za Mamlaka.

TCRA na ustawi wa Watanzania

Katika kufanya kazi zake, Mamlaka inajitahidi kuendeleza ustawi wa jamii ya Tanzania kwa:-

Kukuza ushindani unaofaa na ufanisi wa uchumi

- Kuendeleza upatikanaji wa huduma zilizodhibitiwa kwa watumiaji wote ikiwa ni pamoja na wenye kipato kidogo waliopo vijijini na wateja walio katika mazingira magumu.
- Kulinda maslahi ya watumiaji
- Kuendeleza elimu kwa wananchi kuhusu utambuzi na uelewa wa sekta zilizodhibitiwa ikiwa ni pamoja na haki na wajibu wa watumiaji;namna ambavyo malalamiko yanaweza kuwasilishwa na kutatuliwa na kuhusu majukumu, kazi na shughuli za Mamlaka.